

MKATABA WA UPANGAJI WA FREMU

MKATABA HUU umefanyika hii leo tarehe 02... Mwezi... 02... Mwaka 2025.

BAINA YA

YAKOBO ISAYA YAKOBO wa **DAR ES SALAAM** ambaye ataitwa na kujulikana kama **MPANGISHAJI** kwa upande mmoja.

NA

RALLY LINK COMPANY LTD wa S. L. P. 21879, **DAR ES SALAAM** ambaye katika Mkataba huu ataitwa na kujulikana "**MPANGAJI**" kwa upande wa pili.

Kwa kuwa **MPANGISHAJI** anamiliki kihalali nyumba iliyopo mtaa wa Kichangachui-Kibugumo Mjimwema Wilaya ya Kigamboni Mkoa wa Dar es Salaam.

KWAMBA Mmiliki anapangisha fremu hiyo kwa Mpangaji kwa makubaliano yaliyopo hapa chini.

NA KWAMBA Mpangaji ameridhia kupanga fremu nambari
Katika nyumba hiyo kwa ajili ya biashara na kwa masharti wanayokubaliana.

BASI MKATABA HUU WA FREMU TAJWA UNASHUHUDIA KAMA YAFUATAYO:


1. Kwamba kodi ya fremu hiyo ya biashara ni **Shilingi Eflu Hamsini Tu (Tshs. 50,000/=)** kwa mwezi na mpangaji amelipa kodi ya **Shilingi Laki Tatu (Tshs. 300,000/=)** ambayo ni Kodi ya Miezi Sita.
2. Kwamba Mkataba huu utadumu kwa muda wa Miezi Sita kuanzia tarehe 01/03/2025 hadi tarehe 31/08/2025.
3. Kwamba baada ya mkataba huu kuisha muda wake, Mpangaji anatakiwa kulipa kodi mpya kadri ya makubaliano yao ili kuendelea na mkataba mwingine.
4. Kwamba Upande wowote utakaovunja mkataba bila ya sababu za msingi utawajibika kufidia hasara zozote zitakazojitokeza kwa upande mwingine ambao haujavunja mkataba.

5. Kwamba Usafi, umeme na ulinzi ni jukumu la Mpangaji.
6. Kwamba Mpangaji atahusika na matengenezo ya fremu kama kutakuwa na uharibifu uliosababishwa na yeye mwenyewe au mtu yeyote aliye chini yake katika kipindi cha mkataba huu.
7. Kwamba Mpangaji hatakiwi kupangisha mtu mwingine au kumuuzia fremu mtu mwingine nje ya aliyeingia mkataba na Mpangishaji, ikitokea Mpangishaji amethibitisha hilo atakuwa na uwezo wa kuvunja mkataba muda wowote na Mpangaji kutolewa katika eneo husika.
8. Kwamba Mpangaji atatakiwa kufanya biashara iliyo/zilizo halali kwa mujibu wa sheria za nchi.
9. Kwamba Mpangaji atatakiwa kulipa kodi mwezi mmoja kabla ya mkataba kuisha ikiwa ana lengo la kuendelea na upangaji.
10. Kwamba Makubaliano ya mkataba ni kipindi cha Miezi Sita.
11. Kwamba Mkataba huu uheshimiwe na kuzingatiwa kanuni zake.
12. Kwamba ikitokea kutoelewana au na kutoridhika kuendelea na kumpangisha Mpangaji, mwenye nyumba atatoa notisi ya miezi mitatu kabla ya Mkataba kuisha ikieleza kusudio la kutoendelea kumpangisha au kwa upande wa Mpangaji kutoendelea kupanga.
13. Mwenye nyumba atakuwa na haki ya kurudishiwa fremu yake kama hawatafikia maridhiano.

Makubaliano haya ya mkataba yamefanyika kati ya Mpangishaji na Mpangaji mbele ya Mwanasheria (Wakili).

KAMA USHUHUDA: Pande zote zimekubaliana kwa kuweka sahihi kama ifuatavyo:

IMEWEKWA sahihi hapa Dar es Salaam na
YAKOBO ISAYA YAKOBO ambaye
 namfahamu/ametambulishwa kwangu na
**YUSRA AWADH SAID**.....
 ambaye namfahamu binafsi leo
 hii tarehe ..22... mwezi ...02... 2025



.....
MPANGISHAJI

MBELE YANGU:


JINA: HUSSEIN SAID JUMA
SAHIHI: Haka
ANUANI: S. I. P. 45733, DSM
WADHIFA: KAMISHNA WA VIAPO.



Imetiwa saini kwa niaba ya RALLY LINK COMPANY LIMITED
Leo tarehe 22 Mwezi 02 2025

MUHURI

JINA: YUSRA AWADH SAID
SAHIHI: YUSRA
CHEO: MKURUGENZI



MBELE YANGU:

JINA: HUSSEIN SAID JUMA
SAHIHI: Haka
ANUANI: S. I. P. 45733, DSM
WADHIFA: KAMISHNA WA VIAPO

